

# Rubric - Kara (Tanzania) (Kara)

Original

## 1. Kupima Usahihi

1. Je, tafsiri imewasilisha maana au ujumbe uliokusudiwa bila kuupotosha?
2. Je, tafsiri haijapunguza au kuongeza maana au ujumbe ambao haupo katika lugha ya chanzo?

## 2. Kupima Uwazi wa Lugha

1. Je, tafsiri imetumia maneno yanayoeleweka kwa msomaji wa lugha husika?
2. Je, tafsiri imetumia maneno ya lugha husika yanayoweza kueleweka kwa watu wa rika zote?

## 3. Kupima Uaminifu wa Matumizi ya maneno

1. Je, tafsiri imewasilisha maneno muhimu kwa usahihi?
2. Je, tafsiri ya maneno muhimu inawasilisha maana iliyokusudiwa katika lugha ya chanzo?
3. Je, tafsiri imewasilisha ujumbe usiofungamana na mitazamo ya kidhehebu, kisiasa, kidini, au Kitheologia?

## 4. Kupima Uwasilishwaji wa Mamlaka ya Biblia

1. Je, tafsiri imezingatia nafasi na uongozi wa Roho Mtakatifu?
2. Je, tafsiri imewasilisha ujumbe wenye mguso wa Roho Mtakatifu kwa msomaji?

## 5. Kupima Kujieleza Kwa Lugha/Tafsiri

1. Je, tafsiri imezingatia taratibu za kawaida za uandishi?
2. Je, tafsiri imetumia maneno rahisi, sahihi na yanayoeleweka kwa wasomaji wengi?

## 6. Kupima Uwasilishwaji wa Historia

1. Je, tafsiri imewasilisha matukio ya kihistoria kama yalivyo katika lugha ya chanzo?
2. Je, majina ya watu, mahali au sehemu yamewasilishwa kama yalivyo katika lugha ya chanzo?

## 7. Kupima Uwasilishwaji wa Asili ya lugha

1. Je, tafsiri imetumia misemo au muundo wa uandishi unaoleta uhalisia wa lugha husika?
2. Je, tafsiri imetumia maneno au misamiati inayowasilisha asili ya lugha husika?